**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**
**MPANGO WA RAIS MHE. DKT SAMIA SULUHU HASSAN WA KUONGEZA WATAALAMU BINGWA NA BOBEZI WA AFYA NCHINI KWA MWAKA 2023/2024 *"SAMIA HEALTH SUPER SPECIALISATION PROGRAM 2023/24"***

**Dar es Salaam, Novemba 29, 2023**

**Ndugu Wanahabari;** Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** imeendelea kufanya mageuzi makubwa ndani ya Sekta ya Afya lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za matibabu hasa ya kibingwa na ubingwa bobezi hapa nchini.

**Ndugu Wanahabari;** Katika kufanikisha azma ya **Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** ya kuwa na watalaam wenye ujuzi wa kutosha wa kutoa huduma bora za matibabu hapa nchini, Wizara ya Afya ilijiwekea lengo la miaka mitano (2020-2025) la kusomesha wataalamu bingwa na bobezi wasiopungua 300 kwa kila mwaka wa fedha kupitia Mpango wa Ufadhili wa Masomo wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuongeza wataalam bingwa na bozezi nchini ujulikanao kama **Dkt. *Samia Health Super Specialisation Program***. Jitihada hizo zitaimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi nchini na kupunguza idadi ya wagonjwa watakaopata rufaa za matibabu nje ya nchi. Kupungua kwa wananchi wanaopata rufaa ya kwenda nje ya nchi kupata matibabu kutaipunguzia Serikali gharama kwa huduma hizo kupatikana ndani ya nchi. Aidha, upatikanaji wa wataalam wa afya bingwa na bobezi nchini itawezesha kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi kutibiwa nchini (Tiba utalii) na hivyo kuchangia pato la Taifa.

**Ndugu Wanahabari;** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imepatiwa jumla ya **Shilingi Bilioni 9** kwa ajili ya mafunzo ya wataalamu bingwa na bobezi katika fani mbalimbali za Sekta ya Afya. Fedha hizo ni muendelelezo wa uwekezaji mkubwa unaofanywa na **Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** katika Sekta ya Afya ambapo kwa mwaka jana wa fedha 2022/2023 alitoa Shilingi **Bilioni 8 hivyo kuwepo kwa ongezeko la shilingi Bilioni moja** kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Fedha hizi zitatumika kugharamia mafunzo kwa wataalamu wapya **601** ambao watasoma utaalamu wa ubingwa na ubingwa bobezi wa fani mbalimbali za Sekta ya Afya. Kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024 jumla ya maombi ya ufadhili **810** yaliyowasilishwa na kati ya hayo, waombaji **655** walikidhi vigezo vya kufadhiliwa na waliochaguliwa kwa ajili ya ufadhili kulingana na fedha iliyotengwa ni **601** sawa na **92%** ya waombaji waliokidhi vigezo. Kati ya wataalamu **601** waliochaguliwa kupata ufadhili wa Serikali kupitia Wizara ya Afya, watumishi wa jinsia ya

kiume ni **377 (62.7%)** na jinsia ya kike ni **224 (37.3%)**. Watumishi waliochaguliwa kupata ufadhili katika vyuo vya ndani ya nchi ni **535 (89%)** na nje ya nchi **66 (11%)**.

Aidha, Serikali kupitia Wizar ya afya itatumia fedha hizi kugharamia wataalam wa afya **100** watakaosoma kwa utaratibu wa Seti baada ya kupokea maombi kutoka kwa hospitali husika. Kwa takwimu hizi, kumekuwa na ongezeko la kufadhili wataalamu wanaoomba kusomeshwa na Serikali kutoka **439** mwaka 2022/2023 hadi **701** mwaka 2023/2024.

***Ndugu Wanahabari***, Wizara imezingatia vipaumbele muhimu vya kisekta katika kuhakikisha waombaji wote wanaosoma taaluma za kimkakati na kipaumbele wanapewa ufadhili. Katika kuzingatia hilo, Wizara imetoa kipaumbele kwa wataalamu wanaokwenda kusoma taaluma za afya ya akili, utengamao na tiba shufaa, taaluma za kibingwa kwenye maeneo ya taaluma zote za kibobezi (super-spcecilialization) ikiwemo upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu, upasuaji wa moyo na mishipa ya damu, magonjwa ya figo, saratani na huduma ya mama na mtoto. Pia waombaji wote wenye sifa wanaotoka maeneo ya pembezoni na wanaofanya kazi kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa wataalamu bingwa wamepewa kipaumbele.

**Ndugu Wanahabari;** Napenda kuwatangazia wataalamu wote waliopata ufadhili huu wa mwaka 2023/2024 kwamba wanapaswa **kukamilisha taratibu za kujaza mikataba ya ufadhili kama ishara ya kukubali ufadhili huu.** Muda wa kujaza mikataba ya ufadhili ni kuanzia tarehe **29 Novemba, 2023** hadi **12 Disemba, 2023**. Nakala ya mikataba hiyo inapatikana kwenye tovuti ya Wizara na pia itatumwa kwa barua pepe kwenye anuani za barua pepe walizotumia wakati wa kuwasilisha maombi

**Ndugu Wanahabari;** Ufadhili huu ni kwa ajili ya kulipiwa ada ya mafunzo na posho ya utafiti kwa watakaofadhiliwa ndani ya nchi na kwa wanaoenda kusoma vyuo vya nje ya nchi watalipiwa ada, posho ya kujikimu wakiwa masomoni (**Stipend**), nauli ya kwenda na kurudi pamoja na posho ya utafiti. Malipo ya posho ya utafiti na posho ya kujikimu yatazingatia viwango vilivyopangwa na Wizara.

**Ndugu Wanahabari**; mwisho kabisa nichukue fursa hii kuendelea kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kuwekeza kwenye Sekta ya Afya hususani katika kuendeleza wataalamu bingwa na mabingwa bobezi ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata matibabu ya kibingwa na kibobezi yanayotolewa na wataalamu wetu wa ndani. Uwekezaji huu, utaondoa adha na usumbufu kwa wananchi kwenda kupata matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi nje ya nchi, kuongeza idadi ya raia wa kigeni wanaokuja nchini kwa ajili ya huduma za kibingwa na kibobezi pamoja na kupunguzia Serikali gharama ya kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi kwa ajili ya matibabu.

**Imetolewa na;**

Ummy Ally Mwalimu (Mb)
**WAZIRI WA AFYA**